

HALMASHAURI YA WILAYA KIBITI

MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA OFISI YA
DED KIBITI TAREHE 24/01/2022

WALIOHUDHURIA

JINA	CHEO	NAFASI
1.0 Rudrick Charles	DPLO	Kaimu Mwenyekiti
2.0 Tumainiel.J.Kamnde	HPMU	Katibu
3.0 Arc.Kassim Mponda	DE	Mjumbe
4.0 Salehe Njoma	DLO	Mjumbe
5.0 Anthony Nyange	DCDO	Mjumbe
6.0 Mwl. Zakayo Mlenduka	DEOP	Mjumbe

AGENDA YA KWANZA; KUFUNGUA KIKAO

Kaimu Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuwaasa kuwa makini katika kikao. Pia aliwataafu wajumbe kuwa ndugu Denis Kitali – Mwenyekiti amepata udhuru hivyo kawatakia kikao chema

Kikao kilifunguliwa saa 3:22 Asubuhi..

AGENDA YA PILI; KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 24/1/2022

Katibu wa kikao aliwasilisha agenda zifuatazo kwa ajili kujadiliwa katika kikao kama ifuatavyo;-

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia Agenda za kikao cha Bodi ya Zabuni cha tarehe 24/1/2022
3. Kupokea na kujadili fedha za UVIKO 19 milioni 90,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tatu kwa moja za watumishi wa kituo cha afya Nyamatanga

4. Kufunga kikao.

AGENDA YA PILI; KURIDHIA AGENDA ZA BODI YA ZABUNI ZA TAREHE 24/1/2022

Mwenyekiti alimualika katibu kuwasilisha Katibu kuwasilisha agenda za kikao cha bodi kisha aliwahoji wajumbe kama wanaridhia agenda hizo kuwa agenda sahihi za kikao hicho. Wajumbe wa Bodi ya zabuni wote kwa pamoja waliridhia agenda hizo kuwa agenda sahihi za kikao hicho.

AGENDA YA TATU; KUPOKEA NA KUJADILI MILIONI 90,000,000.00 ZA UJENZI WA NYUMBA TATU KWA MOJA YA WATUMISHI WA KITUO CHA NYAMATANGA

Katibu aliwasilisha taarifa ya ujenzi wa nyumba tatu kwa moja ya watumishi wa kituo cha afya Nyamatanga ambazo ni fedha zilizotokana na mapambambano dhidi ya UVIKO 19 na manunuza haya yatafantika ngazi ya vituo kwa njia ya force account .

MAONI YA PMU

PMU ilipokea taarifa ya ujio wa fedha hizo milioni 90,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tatu kwa moja ya watumishi wa Nyamatanga nakuhaidi kusimamia manunuza hayo kwa mujibu sheria ya ununuza wa umma.

Baada ya majadiliano wajumbe wa bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Wilaya waliazimia yafuatayo;

AZIMIO

Wajumbe wa bodi ya Zabuni wote kwa pamoja walikubaliana na maoni ya PMU kuwa zoezi la michakato ya manunuza ya Umma ikiwa ni pamoja na usimamizi wa karibu na kamati zitakazoundwa ili ujenziuanze mara moja ili ujenzi uende kwa kasi na kwa ufanisi mkubwa.

AGENDA YA NNE; KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kikao kilifungwa
mnamo saa 05.12 asubuhi .

MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA;



SAINI YA MWENYEKITI

Frederick B. CHARLES

JINA LA MWENYEKITI



SAINI YA KATIBU

TUMAINIEL J. KAMNDE

JINA KATIBU

24/01/2022

TAREHE

24/01/2022

TAREHE